**Lishe bora**

Kiwango cha lisha bora ni sawa na kile cha *Lucerne* ya kawaida.

| Sehemu ya mti | Asilimia % ya Protini | Asilimia D.M |
|---|---|---|
| Majani na vitawi | 15-25 | 60-70 |
| Majani changa | 20-30 | 77-82 |

Mti wa *Lucerne* husaidia sana kama chakula kwa mifugo wakati wa kiangazi ikichanganywa na vyakula vingine. Majani yake yana wingi wa Vitamin A na kiwango cha madini ya Sodium, fosforasi na Salfa ni cha chini na kwa hivyo ni bora kuwapa mifugo chumvi ya kuramba.

Majani yanaweza kupewa kuku ili watage mayai ya hali ya juu. Ingawa hakuna viwango vya sumu vilivyo ripotiwa, mifugo huchukua muda kuzoea kula.

**Kiwango cha Mavuno**

Kiwango cha juu zaidi kilichoripotiwa na tani 5 kwa hekta; ambacho kilipatikana nyanda za juu za Ethiopia baada ya miezi 6 ya kukua.

**Ukoaji wa mbegu**

Mbegu huwa tayari wakati wa kiangazi ambapo mifuko inayozihifadhi hupasuka. Ni vizuri kuvuna kabla ya kupasuka ili zikaushwe kwa jua.

Mbegu huwa hazichipuki mchangani kwa miaka mingi, na zikiota huenda zikaliwa na mifugo hivyo basi kuzuia kukua kwake; hadi kukomaa.


**Kenya Agricultural Research Institute**
S.L.P. 57811, NAIROBI.
Simu: 254-20-4183301-20, Fax. 254-20-4183344
Baruapepe: resource.centre@kari.org
Tovuti: www..kari.org

**Watayarishaji:**
Lukuyu, B.A. Muriuki, K na Lukuyu, M.

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

**Mkurugenzi wa Kituo,**
KARI-Muguga South,
S.L.P. 30148-00100
Nairobi
Simu: (066)328801/6 au 2700617
Nukulisi: (066)32348/32884
Baruapepe: narcmuguga@africaonline.co.ke



Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 23 /2008
**Shilingi Ishirini za Kenya**


# Kulisha mifugo kwa kutumia *Lucerne* ya miti



## Utangulizi

Mti wa *Lucerne (tree Lucerne)* ni aina mpya ya mmea wenye chakula cha hali ya juu kwa mifugo; na ambao pia hutumika kwa mapambo, kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa maji au upepo, kurutubisha ardhi na kuni.

## Maelezo

Ni mti ambao hudumisha rangi ya kijani pasipo kujali musimu. Matawi yake huning'inia yakielekea chini.



Majani yake ni laini na huwa ni ya mseto wa rangi ya samawati na kijani. Maua yake meupe hunukia. Mbegu zake huwa ndani ya mifuko mieusi iliyolazwa na kila mfuko hushikilia mbegu kumi za duara ziliolazwa zenye mseto wa rangi ya kahawa na nyeusi.

## Mwinuko wa ardhi na mchanga

### Mwinuko

Hukua kati ya mita 1,000 na 2,000 na kwingineko mita 3,000 za mwinuko wa ardhi kutoka baharini.

Miti iliyokomaa inaweza kuhimili baridi kali lakini miche haiwezi.

### Mvua

Huhitaji mvua ya kati ya milimita 350 hadi1,600 kwa mwaka. Mvua ya milimita 600 ndiyo bora zaidi lakini miti hii hukua kwa mvua ya milimita 200 kwa sababu mizizi yake hupenya kina kirefu ndani ya udongo.

### Udongo

- Hunawili katika udongo wa mchanga na changarawe kwenye iliyoinuka na inayoruhusu maji kuteremka.
- Hudhoofishwa na maji mengi yaliyosakama.
- Hufanya vizuri kwenye michanga yenye kimo cha asidi cha 4.0 na pia mchanga wa alkaline yenye kiwango cha PH 8.5.

## Matayarisho ya miche

Mbegu zinahitaji kuroweshwa kwa maji moto kwa masaa 48 kabla ya kupandwa. Kwa matokeo bora, mbegu hizi zinafaa kutiwa dawa ya *rhizobium*.

### Kitalu cha mbegu

Kinafaa kutayarisha vizuri na magugu ya kila aina kuondolewa.

#### Kupanda mbegu:

- Panda mbegu moja moja katika mashimo ya kina cha sentimita 1 hadi 2.5 lakini zaidi katika sehemu kavu ili mbegu ipate unyevu wa kutosha.

#### Kupanda kwa kitalu

- Mbegu zinaweza kukuzwa kwa kitalu bila kumwagilia maji mengi.

### Kuhamisha miche

- Hamisha miche kwa udongo laini inapofikia urefu wa sentimita 45.
- Panda kwa mistari ya mita 5 na kila kwa mita 2.5 ili miti 700 iweze kutoshea kwa ekari moja.
- Tumia kilo 200 za mbolea ya super phosphate kwa ekari kila mwaka.

## Utunzaji

Zuia mifugo kuchuna ngozi na majani kwa kipindi cha kati ya miaka 2 na 3 kisha unaeza kuliza mfululizo.

Hakikisha miti imeachana kwa mita moja ikiwa inalishwa ng'ombe na mbuzi.

Mti wa Lucerne hukatwa ili ukue tena ingawa huchukua muda kukua tena. Kuvuna miti wakati wa kiangazi husitisha kukua kwake na huenda miti ikakauka.
Miti inaweza kukaa kwa muda wa miaka 30 ikitunzwa vizuri.

**Zingatia:** *Lucerne miti inaweza kuwa shida kama gugu hasa katika sehemu za mvua nyingi.*

### Wadudu adui

Baadhi ya wadudu wanaoharibu lucerne mti ni nondo konokono, na panzi. Sungura hupenda majani yake pia.

### Magonjwa

Ugonjwa mkuu ni kuoza mizizi kunakosababishwa na kuvu na kuweko kwa unyevu uliozidi.

Tatizo hili hupunguza matumizi ya mti kwenye sehemu zenye unyevu mwingi na udongo mzito wa kunata.